# *IMANI*

. . . wimbo huo tena, *Amini Tu.* "Mambo yote yanawezekana, amini tu."

2 Nasi hatuna hapa na—nafasi ya kutosha kuketi tupate kuwa na kanisa letu dogo. Nalo linakaa yapata watu mia kadhaa tu, nadhani, ama zaidi kidogo. Na tunasikitika kwamba inawabidi watu kusimama. Lakini, nitaharakisha, mara moja, na—na matamshi yangu machache ambayo sina budi kutoa. Nami nitaomba ya kwamba Mungu atawapa yote mliyokuja hapa kuona, usiku wa leo, na kuifanya mioyo yenu ijazwe na wema Wake na rehema Zake. Kwa maana kweli najua ya kwamba hayo yangekuwa ndiyo mapenzi Yake ya Kiungu, kwamba iwe hivyo.

3 Jambo la kwanza ninalotaka kusema, ya kwamba tutamkumbuka kwa hamu ya kutaka kumwona kwa muda mrefu hapa, kuondoka kwa Dada yetu Casey. Ingawa ni mzee, nafikiri, katika miaka yake ya mbele sana ya themanini, na huku siku baada ya siku katika theluji na mvua, alipokuwa akienda zake kwenye kanisa la Mungu aliye hai. Hivi majuzi usiku ilikuwa ni majaliwa makuu kusimama kando ya kitanda chake alipokuwa akiaga. Nami nikasema, "Unanijua?" Naye. . . Sijui kama alinijua au la. Lakini niliposema, "Je, unamjua Yesu?" Alitikisa kichwa chake, ndiyo, kwamba alimjua. Ndipo nikafurahia kuwaita watoto wake, wajukuu wake, pia, naamini, hata vilembwe, karibu na kitanda, na kusema, "Hiyo ndiyo njia ya kuaga."

4 Hata hivyo, hatuna budi kwenda. "Mtu amewekewa kufa mara moja, na baada ya hapo hukumu." Na kisha Dada yetu Hall. . .

5 Ndugu William Hall, mchungaji wa kanisa la Kibaptisti la Milltown, ambaye alikuwa ni mwongofu kwa Bwana, katika mojawapo ya ile mikutano hivi majuzi, miaka michache iliyopita, naye aliponywa kansa hatari sana. Wakati madaktari waliposema, walio bora zaidi ambao wangepatikana katika sehemu yake ya nchi, halafu basi daktari wa New Albany akasema, "Yuafa." Naye akaja hapa. Naye mkewe. . . akanipigia simu, akasema, "Ndugu Billy, utakuja kumwombea Will? Yuafa kwa kansa." Nasi tukashuka kwenda kumwona. Nayo hiyo kansa ilikuwa ya ini, nayo ililivimbisha ini lake sana, naye akageuka manjano na karibu apoteze fahamu. Nami nikamwuliza kama angejali nikimwita daktari rafiki yangu hapa mjini, aongee na yeye. Huyo alikuwa ni Daktari Sam Adair. Wengi wenu mnamfahamu.

6 Naye Daktari Sam akasema, "Billy, kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni kumpeleka Louisville, kwa mtaalamu fulani

maarufu wa kansa." Ndipo wakampeleka kule akafanyiwe uchunguzi. Na, bila shaka, daktari kule asingemwambia, kwa hiyo akampigia simu Daktari Adair. Naye Daktari Adair akanipigia simu, naye akasema, "Billy, mhubiri rafiki yako atakuwa amekufa katika siku nne." Kasema, "Yuna siku nne zaidi za kuishi," kasema, "kwa sababu kansa imekula ini lake kabisa."

Nikasema, "Daktari, je, hakuna unachoweza kumfanyia?"

7 Akasema, "Billy, tusingeweza kutoa ini lake, na aishi." Kisha akasema, "Ikiwa yeye ni mhudumu, anapaswa kuwa tayari kwenda."

Nikasema, "Hilo, ninaamini yuko tayari."

8 Kwa hiyo lilikuwa jambo gumu kwangu kwenda kumwambia mke wake mpendwa kwamba Ndugu Will Hall atakuwa amekufa katika siku nne. Familia ya Wright hapa, inayoketi hapa, ambapo wao ni mashahidi wake, na wengine wengi zaidi. Na ambapo . . . Nilishuka na kumwambia Bibi Hall, "Will atakufa ndani ya siku nne. Daktari anasema ini lake limeliwa na kansa." Kwa hivyo nikaja nyumbani.

9 Basi kesho yake asubuhi . . . Watu wengi huja nyumbani, mwajua, nami inanibidi kutoka kwa muda kidogo tu. Ndio kwanza nitoke kwenye safari kama hiyo, kule chini Kentucky ambako nilikuwa nikiwinda. Nami nilikuwa naenda kuwinda kuchakulo asubuhi hiyo. Nikaingia mapema, na kuchungulia nje, wala hapakuwapo na mtu kwenye njia ya kuingia nyumbani. Kwa hiyo ni—nikaenda na kuchukua kofia yangu kuukuu na bunduki ya .22, nikaanza kutoka.

10 Ndipo nikaona tofaa limening'inia pale, lilikuwa ni to—tofaa lenye sura ya kuchukiza zaidi nililowahi kuona. Nikawazia, "Je, Meda aliweka aina hiyo ya tofaa ukutani kwa nini?" Lenye vifundo na limeliwa na wadudu. Ndipo nikaona kuwa halikuning'inia ukutani. Lilikuwa hewani. Nami nikapiga magoti huku nimeishika kofia yangu kuukuu na bunduki mkononi mwangu. Kisha nikaona tofaa lingine, na tofaa lingine, mpaka matofaa matano yakasimama pale. Kisha tofaa lingine kubwa mno lenye milia myekundu ndani yake, likashuka na kufanya ming'wafuo mikubwa mitano, na kukata tu hayo matofaa vipande vipande na kuyameza. Nami nikawazia, "Ni nini hii?"

11 Ndipo Malaika wa Bwana, ambaye picha yake mnaiona pale, akasimama chumbani na kusema, "Nenda ukamwambie Ndugu Hall, BWANA ASEMA HIVI. Hatakufa. Amekuwa mgonjwa miezi mitano sasa, lakini ndani ya siku tano atakuwa mzima."

12 Haraka, nikampigia simu Daktari Adair, nami nikasema, "Ataishi."

13 Akasema, “Billy, anawezaje kuishi na ini lake limeliwa likaisha?”

14 Nikasema, “Sijui. Lakini Bwana alisema tu kwamba ataishi, na hilo ndilo tu nijualo.” Naye yu hai leo.

15 Naye mkewe, nadhani karibu umri wa miaka sabini na mitano ama themanini, aliponyoka akaenda kuwa pamoja na Bwana, siku chache zilizopita, nilipokuwa huko Kentucky. Mungu aipe raha nafsi yake, na Dada Casey, pia. Wote wawili wamekuwa katika kanisa hili na kushiriki pamoja nasi.

16 Kila mwanadamu, haijalishi ni mchanga au mzee vipi, au yuna afya jinsi gani, ipo siku moja ambayo sote tutakutana na Mungu. Tunaweza kujiandaa kwa ajili ya hilo.

17 Sasa, usiku wa leo, mimi. . .maneno machache tu kutoka kwa Neno la Milele na lililobarikiwa la Mungu. Nami ningetaka kusoma sehemu Yake hapa, inayopatikana katika Kitabu cha Marko Mtakatifu, katika mlango wa 11 wa Marko Mtakatifu. Ninataka kuzungumza juu ya *Imani*, kwa dakika chache tu, maana wengi wenu mmesimama, viungo vyenu vitakakamaa. Ninataka kuanzia kwenye kifungu cha 20. Ninataka kuisoma kutoka katika kamusi ya msamiati ya Kiyunani.

> *Basi asubuhi walipokuwa wakipita, waliuona ule mtini umenyauka toka mizizini.*
>
> *Petro akakumbuka habari yake* akamwambia, *Mwalimu, tazama, mtini* ulioulaani *umenyauka.*
>
> . . . *Yesu akajibu,* akawaambia, *Mwaminini Mungu.*
>
> *Kwa maana, amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'o-. . .ng'oka . . . ukatupwe baharini; wala asione shaka moyoni mwake, ila . . . aamini kwamba mambo hayo asemayo* yatatukia; *yote asemayo yatakuwa yake.*

18 Ni ahadi yenye baraka jinsi gani! “Kumwamini Mungu!” Ni jambo la kushangaza mno kwa watu wengi. Na, hata hivyo, tunapaswa kujionea aibu, kukiri ya kwamba hatumwamini Mungu.

19 Kwanza, kuna waoga ambao hufa vifo elfu kumi, wakati wakiwa hapa duniani, wala shujaa hafi kamwe. Kumbukumbu zake hudumu kwa ajili ya matendo yake makuu ya kishujaa.

20 Na, kwa kawaida, watu walio na imani ni watu ambao wana ujuzi. Ujuzi huleta imani. Nafikiri hiyo ndiyo sababu Biblia inatufundisha . . .

21 Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 3, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuelewa ufalme wa Mungu.” Sasa, hiyo ni kunukuu kutoka kwa la asili. Katika la—la King James, lilisema, “Hawezi *kuona*.” Lakini hilo neno halimaanishi “kuona,” kama vile unavyoangalia kwa macho

yako. Linamaanisha kuelewa. Huwezi kuuona ufalme, kwa vyovyote vile. Huna budi kuuelewa. Naye Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, kwanza, ataninii . . . hawezi kuuelewa ufalme wa Mungu." Kwa hivyo ni . . .

22 Inatubidi kuwa na tukio kabla imani haijaweza kutimiza mengi sana. Kwa hivyo, watu wanapaswa kuokolewa kabla . . . kwanza, wamjie Mungu na kupata tukio la wokovu, kabla ya kumkaribia Mungu kwa ajili ya uponyaji wao. Ni lazima . . . Ita—itafanya maajabu, ikiwa unaweza tu kuamini.

23 Sasa angalieni, mara nyingi, katika Maandiko. Hebu tuchukue mandhari maarufu ya kale ya Israeli, wakati walipokuwa katika shida. Basi vita vikatokea kati ya Israeli na Wafilisti, nao Israeli walikuwa wamekusanyika kando ya kilima. Basi vita vikapangwa, lakini hakuna mtu aliyeweza kwenda vitani, kwa sababu, upande wa pili wa kilima, adui alikuwa na mpinzani mkuu.

24 Na kama ilivyokuwa wakati huo, ndivyo ilivyo sasa, kwamba, watu wa Mungu wanapoanza kwenda kufanya jambo fulani, adui daima huwa na mpinzani; anakupa changamoto yake.

25 Basi hili jitu kubwa mno, karibu la kabla ya historia, lilisimama pale likiwa na vidole vya inchi kumi na nne. Na mkuki mkononi mwake, ukubwa wa sindano ya mfumaji. Alimpa changamoto mwanamume yeyote wa Israeli aje apigane naye.

26 Hivyo ndivyo adui afanyavyo, anapofikiri anaweza kukushinda. Hatawahi kufanya hivyo anapoona imani inayoshinda. Lakini atafanya tu wakati anajua kuwa amekuogopesha. Hapo ndipo Kanisa haliwezi kusonga mbele, ni wakati amekuwekelea sindano ya mfumaji.

27 Lakini, wakati, katika majeshi ya Waisraeli, Sauli, yule shujaa mkuu . . . Ikiwa kulikuwa na mtu yeyote katika jeshi lote ambaye alifaa zaidi kwenda kupigana na jitu hili, alikuwa ni Sauli. Kwanza, alikuwa shujaa aliyefunzwa vizuri. Alijua ujanja wote, jinsi ya kukwepa mikuki, na jinsi ya kuipiga kumbo kwa ngao yake. Na zaidi ya hayo, kichwa chake na mabega yake alikuwa mrefu kuliko mtu yeyote jeshini mwake. Kimwili alikuwa mshindani bora zaidi, na alikuwa mkufunzi wa wanaume.

28 Lakini kama ilivyokuwa kwa Sauli, katika siku hizo, tunaona jambo lile lile likiwapo siku hizi, miongoni mwa watu wanaoenda kanisani. Baadhi yao ambao ni wasomi waliofunzwa vizuri zaidi, wana imani duni sana kwa Mungu, wakati mwingine. Wana Ph.D na ma-D.D., na wanajaribu kulielezea . . . Ama, kujaribu kujiepusha na ukweli wa kukabiliana na Neno la Mungu, wanajaribu kulielezea vinginevyo, kwa njia nyingine. Na ni kweli. Usomi wetu wote, mafunzo yetu yote, kamwe

hayatuweki katika hali ya kukutana na adui. Inahitajika kumwamini Mungu, kufanya hivyo, na hivyo pekee. Lakini kama tukiangalia, wakati jitu hili lilipokuwa likijivuna sana. Naye mwanatheolojia huyu mashuhuri, tuseme, akasimama pale, amefunzwa vyema kujua jinsi ya kupigana, lakini kamwe hakuwahi kupata tukio lolote na Mungu.

29 Na inasikitisha sana, siku hizi, kuona wanaume na wanawake, ambao wameishi kanisani, wameletwa katika kitanda hiki cha mtoto, nao wanajua Biblia vizuri, lakini bado hawajawahi kushuhudia tukio na Mungu. Tunachohitaji ni kurudi kwenye tukio la kweli la kuhisiwa moyoni, ili kumjua yule unayemwamini. Si maandishi fulani, bali Mungu wa kweli na aliye hai Ambaye anaishi sasa.

30 Na hapo katikati ya hayo, kule nyuma kabisa, nyuma ya mashamba, Mungu alikuwa na mvulana mdogo mwekundu, jina lake Daudi. Alichunga baba yake—kondoo wa baba yake. Ndipo alipokuwa akichunga kondoo wake, alipata tukio fulani. Na baba yake ndiye aliyemtuma kwa jeshi, kuwapelekea ndugu zake mikate ya mtini na keki za zabibu kavu. Basi alipokuwa kule juu, aliona jitu hili kubwa likitoka na kutoa majivuno haya makubwa ya kiwazimu.

31 Sasa, maskini Daudi hakuwa mshindani wake hata kidogo. Kwanza, alikuwa ni jamaa mdogo tu. Na jambo la pili, alikuwa jamaa *mwekundu*, maana yake alikuwa “maskini kibete,” jinsi tungemwita. Wala hakufaa hata kidogo. Hakuwahi kushika upanga mkononi mwake, pengine hakuwa amewahi kuitwaa ngao, maishani mwake. Hakujua lolote kuhusu mafunzo ya kijeshi.

32 Lakini kuna jambo moja alilojua. Alimjua Mungu wake. Hilo ndilo jambo kuu. Alimjua Yule aliyekuwa amemwamini. Na hivyo wakati lile jitu lilipotoa changamoto yake, Daudi alijua jambo lingine: mema na mabaya.

33 Wakati mwingine, sisi tunaoenda kanisani, haionekani kama hata tuna akili ya kiroho kujua tofauti. Endapo tunayo, hatutendi vinginevyo.

34 Lakini alijua mema na mabaya. Alijua ilikuwa ni makosa kwa Mfilisti huyo kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai. Basi akasema maneno haya, “Mnataka kuniambia, kwamba mtamruhusu huyo Mfilisti asiyetahiriwa asimame hapo na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai?” Ni shutuma la jinsi gani kwa jeshi lililofunzwa!

35 Ni shutuma la jinsi gani, leo, kwa maskini dobi mwanamke, labda, asiyejua ABC zake, lakini anaweza kusimama mbele ya kasisi aliyefunzwa vyema ambaye anasema siku za miujiza zimepita, na kuyakaidi maneno yake, kwa kusema, “Wakati mmoja nilikuwa kilema, au mgonjwa, na sasa nimepona.”

Huenda asijue mambo yote ya ndani na nje ya theolojia, bali anamjua Mungu. Hata hivyo, hilo ndilo linalohitajika.

36 Na hapo maskini Daudi huyu mwekundu, kijana tu aliyevikwa kanzu yake ndogo ya kondoo, alitembea mbele ya watu hao na kuwafanya wajionee aibu. Kisha akasema, "Mnasimama hapo, jeshi lililofunzwa la Mungu aliye hai, na kumwacha Mfilisti huyo ayatukane majeshi ya Mungu." Kasema, "Nitakwenda kupigana naye, mimi mwenyewe." Loo, ninaipenda roho hiyo ya ujasiri ndani ya Daudi.

37 Naye Sauli akajaribu kumsomesha, na kumvika koti la kikanisa, lakini halikumwenea. Akasema, "Ondoeni kitu hiki kwangu, sijui jinsi ya kusema 'ah-amina' jinsi msemavyo. Na wala sijui theolojia zenu. Acha niende na kile ambacho nina ujuzi wake."

38 Loo, jamaa fulani aliniambia wakati fulani uliopita. Akasema, "Ndugu Branham, mahubiri yako ni bure, kwa maana hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu."

39 Nikasema, "Jambo moja ndilo hili, ndugu. Kamwe hujawa mahali ambapo tumetembelea. Hivyo tu. Maana umechelewa kupita kiasi kutwambia sasa. Tayari tumeupata na kuushuhudia, duniani kote, ule uamsho mkuu wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, kuleta ishara na maajabu, kulitimiza Neno la Mungu katika siku hizi za mwisho."

40 Ndipo maskini jamaa huyu akaondoa digrii hizi za kale kutoka kwake, akatoka hapo, naye akasema, "Angalieni hapa, hii ndiyo sababu ninapanda kwenda huko. Ninamjua Yule niliyemwamini."

41 Sauli hakujua lolote kuhusu hilo, ingawa alienda kanisani kila sabato. Naye huenda alifanya mambo yote ya kidini ambayo hao wengine walifanya, lakini hakuwahi kupata ujuzi.

42 Basi ilikuwaje? Daudi akasema, "Nilipokuwa nikichunga kondoo wa baba yangu, huko nje nilipopita kwenye malisho ya majani mabichi, na kando ya maji matulivu, nilipata kumjua Mungu aliyeziumba mbingu na nchi. Nami niliwajibikia kondoo wachache wa baba yangu. Ndipo dubu akavamia na kumkamata mmoja, nami nikamwua. Kisha simba akavamia na kumshika mwana-mbuzi, na kutoroka, nami nikambwaga chini kwa kombeo langu. Ndipo alipoinuka, nikamshika ndevu zake na kumwua." Akasema, "Mungu aliyeniokoa na dubu pamoja na simba, ni zaidi sana jinsi gani atamtia Mfilisti huyo asiyetahiriwa mikononi mwangu." Bila shaka, alijua alichokuwa anazungumzia. Alimwamini Mungu. Alikuwa na ujuzi, kuona kile ambacho Mungu angefanya, kwa hiyo alijua tukio hilo lingempeleka kwenye ushindi.

43 Loo, miaka mingi baadaye, wakati alipokuwa mfalme wa Israeli. Hapana shaka kwamba alifanywa mfalme, kwa shujaa kama huyo. Alipokuwa mfalme, alikuwa na wazo, "Acha niijenge

nyumba ya Bwana.” Ndipo wakati nabii Nathani, usiku ule, alipomtoa nje na kuzungumza naye.

44 Bwana alimtokea Nathani. Akasema, “Nenda ukamwambie mtumishi Wangu, Daudi, najua alikuwa tu kitu kidogo chekundu. Najua alikuwa anavaa koti la kondoo. Lakini nalimtoa katika zizi la kondoo, na kumfanya kuwa mkuu juu ya watu Wangu, na kumpa jina kama watu wakuu katika dunia hii.” Jinsi Mungu aliona unyofu huo wa imani kumwamini, juu ya tukio la kwamba Yeye alikuwa Mungu aliye hai.

45 Jinsi ilivyokuwa kidogo kwa Ibrahimu, baada ya kuvumilia kama kumwona Yeye asiyeonekana. Jinsi, baada ya kukutana na Mungu, na kupata ujuzi wa kuzungumza ana kwa ana na Mungu, ili aweze kuviita vitu ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwako. Kwa maana, alikuwa na ujuzi. Alikuwa amezungumza na Mungu, ana kwa ana. Hilo ndilo tunalohitaji, ni ujuzi wa kibinafsi na Mungu aliye hai.

46 Jinsi Musa, baada ya kuwa na miaka arobaini ya mafunzo ya dini na mama yake, jinsi akiwa na miaka arobaini ya nguvu za kijeshi mikononi mwake, jinsi ya kupiga taifa, jinsi ya kushinda, nayo ilimchukua Mungu miaka arobaini kuiondoa kwake. Lakini akiwa huko nyikani peke yake, siku moja, alikutana na Mungu uso kwa uso, kwenye kichaka kilichowaka moto. Naye alihamasishwa vizuri zaidi, katika dakika tano, baada ya kuzungumza na Mungu, kuliko vile miaka themanini ya masomo ilivyokuwa imemfanyia chochote. Alikuwa mwoga, akifa vifo elfu moja. Ndipo baada ya kukutana na Mungu, alitamani angekuwa na maisha elfu moja ya kufa, kwa ajili ya Kristo. Alikuwa tayari kwenda. Hakuna kitu ambacho kingeweza kumzuia, ingawa hakuwa na jeshi, ingawa elimu yake haikuwa nzuri kwake. Hakuweza kupigana; hakuwa na panga. Hakuwa na wapiganaji wowote, magari yoyote ya vita ya kumuunga mkono, kadiri ulimwengu ulivyojua. Lakini alikuwa amekutana na Mungu uso kwa uso, akiwa na ujuzi, ambaye alikuwa na Malaika wenye silaha wa Umilele wote kusimama nyuma yake. Basi Musa alipokuwa akienda zake, akishuka pamoja na mkewe, akiwa ameketi kwa kutagaa juu ya nyumbu mdogo, huku masharubu marefu yakining’inia, ninaamini ya kwamba elfu kumi mara elfu kumi ya Malaika waliambatana naye, wakishuka kwenye barabara hizo zenye mavumbi pamoja naye. Alikuwa na ujuzi.

47 Ilikuwa kule Dothani, wakati mmoja, wakati kijana mmoja, m—mtumishi wa nabii, basi akashuka pamoja naye mpaka Dothani. Naye nabii alipokuwa amelala, jeshi kubwa la Washami lilikuja na kuwazingira, likapiga kambi kuzunguka kuta kubwa za Dothani. Basi alipoamka, kesho yake asubuhi. . .Hakuwa amepata kuwa na ujuzi. Akasema . . . alipoliona lile jeshi kubwa, likimtafuta Eliya, akasema, “Loo, baba yangu, majeshi yote yamekusanyika na kutuzingira hapa. Wanakutafuta.”

48 Haikumshtua nabii huyo mzee, hata kidogo. Huenda ilikuwa ni kansa, huenda ikawa ilikuwa ni kifua kikuu, huenda ilikuwa kiharusi, lakini haikumshtua nabii huyo. Akamtazama, naye akasema, “Mwanangu, kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.”

Alisema, “Ninaweza kukuona wewe na mimi tu.”

49 Akasema, “Yafumbue macho yake, Mungu, apate kuona. Mpe ujuzi.” Ndipo wakati macho yake yalipofumbuka, alitazama, na milima yote imejaa magari, na moto, na farasi wa moto, karibu na yule nabii mtakatifu mzee. Alikuwa na ujuzi. Hakukuwako na shaka tena akilini mwake wakati huo.

50 Ilikuwa ni Samsoni akiwa na taya ya nyumbu, aliyewaua Wafilisti elfu moja, kwa sababu alikuwa na ujuzi, kwamba alizaliwa mara ya pili. Alikuwa na ujuzi, ya kwamba alikuwa Mnadhiri, na Mungu wa Mbinguni alikuwa pamoja naye.

51 Ilikuwa ni Filipo ambaye alikuwa amemwona Yesu, katika matukio ya awali, ambaye alikwenda na kumkuta Nathanaeli karibu nyuma ya mlima. Naye akasema, “Njoo, umwone tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

52 Naye mtu huyo, akiwa ni Mworthodoksi, alisema, “Sasa, jambo jema laweza kutoka Nazareti?”

53 Akasema, “Njoo uone.” Kwa nini? Alikuwa pamoja na Yesu. Alijua kwamba kulikuwa na kitu kuhusu Mtu huyo, kilichokuwa ni zaidi ya mshindani kwa kitu chochote ibilisi angeweza kustahimili. Loo, sikilizeni kwa makini.

54 Basi walipouzunguka mlima, Filipo anaanza kuzungumza, naye Nathanaeli anazungumza naye. Naye akamwambia, “Sasa, ukifika huko. . . Nimemwona. Wakati Petro alipokuja, na Yeye hata (kamwe) hakumwona Petro, maishani Mwake mwote. Lakini alipofika kule, Yeye akasema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Alijua jina lake, naye alijua baba yake alikuwa nani.” Loo, asingeweza kuamini hilo. Lakini Filipo alikuwa amewahi kuwa pamoja Naye, kwa hiyo alijua kumshawishi, jinsi ingeweza kuwa, jinsi alivyofanya jambo hilo.

55 Kwa hiyo alipopanda Mbele za Yesu wa Nazareti, alikuwa amekuja basi kuamini. Ndipo alipomtazama, alimwambia; akasema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Naye akamwambia, “Ulinijua lini, Rabi?”

56 Naye akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

Sasa, ilimshangaza mno. “Angewezaje kufanya jambo hilo?”

57 Lakini, Filipo alijua kwamba, ili kumshawishi Nathanaeli, kwamba lingeweza kufanyika, kwa sababu alikuwa ameshapata ujuzi wa kuwa pamoja na Yesu.

58 Mnajua, kuna kitu kuhusu kuwa pamoja na Yesu, hukupa ujuzi. Kuwa karibu na mahali alipo Yeye, kuitazama kazi Yake, ndipo basi hiyo inakupa imani. Unapokuwa na ujuzi, inakupa imani. Imani huendana na ujuzi wako.

59 Sasa naona hili, sasa, wakati akija, vema, tunaweza kuwaona wanapoanza kusemezana huku wakikwea. Naye akaanza kumwambia yaliyokuwa yakitukia, na kwamba yeye alikuwa ni nani na alitoka wapi, na yote kuhusu hilo. Halafu basi mara alipopata huo ujuzi . . . Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Alipopata huo ujuzi, kwamba mwujiza wa Mungu ulikuwa umefanyika juu yake, ndipo angeweza kuanguka miguuni Pake, na kusema, "Rabi, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu aliye hai. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli." Lakini kwanza ilibidi aone likifanyika. Angeweza kumwamini Mungu, baada ya Mungu kujidhihirisha Mwenyewe. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo.

60 Mwanamke ambaye Ndugu Neville alikuwa akisoma habari zake, usiku wa leo, katika Biblia, alikuwa ameketi kisimani, ama akiteka maji kisimani. Alikuwa Msamaria. Alikuwa amefundishwa kwamba atakuja Masihi ambaye angefanya ishara na maajabu makubwa. Alijua kidogo habari zake. Basi walipoichovya ile ndoo kisimani, ili kuteka maji, Yesu alisema, "Nipe maji ninywe."

61 Naye akasema, "Mbona, huna kitu cha kutekea. Na kwa nini uniombe maji unywe? Kwa kuwa Wewe ni . . . Msamaria, kwanza, hatuna uhusiano."

62 Na kadhalika, mazungumzo yakaendelea. Muda si muda, haya ndiyo yaliyotukia, Yeye alipata shida yake. Kumbukeni, yeye kwanza alikuja kule kumkosoa, kama Myahudi. Lakini akasema, "Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa."

Akasema, "Sina mume yeyote."

63 Kasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, naye uliye naye sasa siye mume wako."

64 Na upesi, mara tu hilo lilipotokea, alitatizika akilini mwake. Kumbukeni, alikuwa ameenda kwenye kanisa baridi, la kawaida. Hakujua la kufanya. Akasema, "Vema, sasa, Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Kwamba, tunajua ajapo Masihi, ya kwamba atatwambia mambo haya."

65 Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye." Loo, ni ujuzi ulioje! "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

66 Basi yeye alisema nini? Alikimbia mjini, akiwa na tukio ambalo alikuwa ameshuhudia, kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu aliye hai. Kwa nini? Alikuwa ameona nguvu zikifanya kazi ndani Yake, ambazo zilikuwa zimefanya mwujiza, ambazo zilimwambia yeye alikuwa nani, na dhambi yake ilikuwa wapi, na mahali shida yake ilipokuwa. Kwa hivyo, angeweza kukimbia na kusema, "Kweli, huyo ni Mwana wa Mungu. Njoni, mwone

Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?"

67 Sasa angalieni tena. Katika dakika chache. . .Walikuwa na mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu. Alilia, na kujaribu kila kitu cha kufanya, apate kupona; asingeweza. Alipita katikati ya umati na akagusa upindo wa vazi Lake, kwa maana aliamini. Sasa nini? "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu." Akapenya, kwa maana imani huja kwa kusikia. Akaligusa vazi Lake. Naye akasema, "Hilo linaniridhisha. Nimemgusa." Naye anarudi kwenye umati, akiamini moyoni mwake kwamba jambo fulani lingetukia. Loo, laiti watu siku hizi wangeweza tu kupata hilo, kuamini!

68 Basi lilipotukia, Yesu aligeuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

69 Naye Petro akasema, "Wote wanakugusa. Kwa nini unasema, 'Ni nani aliyenigusa?'"

70 Akasema, "Lakini nimekuwa dhaifu. Mimi ni dhaifu sana! Uweza, nguvu zimenitoka. Mimi ni dhaifu."

Naye akasema, "Vema, ulijuaje jambo hilo?"

71 Naye akatazama pande zote, kwenye huo umati. Alifikiri alikuwa amefichika. Alikuwa huko nyuma, amejificha kwenye umati. Ndipo Yesu alipogeuka na kumwangalia, alimwambia shida yake ilikuwa nini, na ya kwamba alikuwa ameponywa. Na ndipo ikawa, kwamba angeweza kuanguka chini miguuni Pake na kukiri mambo yote. Baada ya kupata tukio la nguvu Zake kuu mno, kumfunulia kwamba alikuwa ameligusa hilo vazi, sio Lake tu, bali la Yeye aishiye milele, Mungu Mwenyezi. Bila shaka, lilikuwa hivyo.

72 Sasa, ilikuwa ni wale watu katika ile Siku ya Pentekoste, ambao walikuwa waoga, nao walikuwa katika chumba cha juu. Milango yote ilikuwa imefungwa. Waliwaogopa Wayahudi. Lakini Mungu alipokuja, katika umbo la Roho Mtakatifu, na kubatiza kila mmoja wa kundi hilo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto, ndipo walipoweza kuingia mtaani. Naye mtu yule aliyelaani Mbele za Yesu, siku chache hapo kabla, angeweza kusema, "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu, Watu hawa hawakulewa kama mnavyodhani, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana, lakini hili ndilo lile lililonenwa na nabii Yoeli." Bila shaka, baada ya kupata tukio! Kabla hajapata tukio, alikuwa na imani ya kuliamini; lakini baada ya hilo tukio kuja, hilo tukio lilileta matokeo. Hakika, lilileta.

73 Sasa, wale watu ambao Yesu amezungumza nao, pale, kuhusu ule mti. Sasa angalieni, kwa muda kidogo sasa, tunapofunga. Alipokuwa anakuja kwenye. . .akitoka hekaluni siku moja. Aliuendea mbio mti mmoja, aone kama wangeweza kupata kitu cha kula, kwenye mti huu. Hakukuwa na kitu kule,

kwa sababu wakati wa tini ulikuwa haujafika. Wala hakupata kitu, kwa hiyo akauambia huo mti, "Tangu sasa hakuna mtu atakayekula kutoka kwako. Hakuna mtu alaye." Ndipo kesho yake . . .

74 Kamwe hawakuona tofauti yoyote kwenye huo mti, papo hapo. Haukuonyesha matokeo yoyote, matokeo yoyote ya kimwili. Sasa hapa ndipo ninapowataka mlipate. Haukuonyesha matokeo yoyote. Lakini Yeye alisema nini? "Hakuna mtu atakayekula kutoka kwako."

75 Na katika muda wa saa ishirini na nne, yapata saa sita mchana kesho yake, walipita karibu na mti ule ule. Na mle ndani, wakaona ya kwamba huo mti ulikuwa umeanza kunyauka. Petro akasema, "Tazama, ule mti ulioulaani, umeanza kunyauka tangu mizizini."

76 Sasa, angalieni yale Yesu aliyosema sasa, tunapofunga. "Mwaminini Mungu." Ati nini? Aliwaonyesha uweza Wake, kwanza. Aliuonyesha juu ya mtini, yale ambayo angeweza kufanya. Kwa sababu, alipomwomba Baba chochote, aliamini kwamba alipokea kile alichoomba. Kisha akawaambia, "Mwaminini Mungu. Kwa maana nawaambia, mkiuambia mlima huu, 'Ng'oka, uinuliwe ukatupwe baharini,' wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba mambo hayo uliyosema yanatimia, yatakuwa yako." Mnalipata? Hili hapa katika kamusi ya msamiati ya Kiyunani, mnaona. "Amini kwamba unayosema yatatimia, yatakuwa yako. Mwamini Mungu. Amini kwamba yale uliyoomba, utayapokea, amini tayari yametendeka, na yatakuwa yako."

77 Sasa, kuhusu "mlima" kuhamishwa. Labda chembe moja ndogo ya mchanga imeanza kusogea, lakini, kwa vyovyote vile, machoni pa Mungu, ilikuwa tayari imetukia. Kama utaamini, usiku wa leo, kwamba, haidhuru una shida gani, kama utaamini unapomwomba Mungu, kwamba unapata kile unachosema, kitakuwa chako. Mwamini Mungu.

78 Lakini, kwanza, Mungu hana budi kujithibitisha Mwenyewe kwako, ya kwamba Yeye—Yeye angali ni Bwana Mungu yeye yule. Angali ni Yehova yeye yule mwenye nguvu. Sasa, Yesu alisema, "Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya."

79 Sasa, kwenu ninyi hapa, usiku wa leo, humu maskanini, tunapoanza kupanga mstari wa maombi, ni wangapi wenu wangesema hivi: "Kama ningeweza kumwona Yesu Kristo akifanya miujiza ile ile, na kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani, Mimi, moyoni mwangu, ningemkubali Mungu, na kuamini kwamba shida yoyote niliyo nayo, ingetukia, mara tu nitakapomwomba Mungu"? Je, ungeamini? Je, waweza kuinua mkono wako? Useme, "Mungu, nitaamini kwa yote . . . " Haijalishi ni nini.

80 Sasa, hakuna mtu anayeweza kuponya. Uponyaji ni bidhaa iliyokamilika ya Mungu. Kama mtu yeyote akikwambia kwamba anaweza kukuponya, kama yeye ni daktari na anaweza kukwambia kwamba anaweza kukuponya, amekosea. Kwa maana, kuna mponyaji mmoja tu, huyo ni Mungu. Daktari anaweza kutoa dawa. Anaweza kuweka dawa kwenye kidonda, ili kuua vijidudu ndani yake, kipate kupona. Inakuwaje? Hiyo dawa haiponyi. Dawa huzuia tu vijidudu vibaya, huua vijidudu vibaya vinavyoua vijidudu vizuri, vinavyokuua. Kwa hiyo, sayansi inafanya kazi kwa sumu mbalimbali ambazo wanaweka mwilini mwako, ili kutia sumu vijidudu fulani, ambayo haitakudhuru. Hivyo ndivyo sayansi inavyofanya. Hivyo ndivyo tiba ilivyo, ni kitu kitakachoua kijidudu fulani, wala hakitakuua. Hivi viuavijasumu huua wote wawili, kwa kiwango kikubwa sana, hivyo basi wao. . . Hiyo ndiyo sababu ni vigumu kuvinywa, kama vile penisilini, wakati mwingine inamwua mtu.

81 Sasa, daktari anaweza kuhamisha kizuizi. Anaweza kuweka mfupa pamoja, lakini hawezi kuponya. Mungu Ndiye aponyaye. Mungu hutoa kalisi. Mungu huleta ku—kuzidishwa kwa seli, kuujenga mwili wako tena, ambapo wameondoa kidole tumbo au kitu kama hicho. Mungu ndiye mponyaji pekee.

82 Sasa, Yesu aliahidi kwamba atatuponya. "Mkiomba lolote katika Jina Langu, nitalifanya. Mwombapo, aminini ya kwamba mnayapokea yale myaombayo, yatakuwa yenu." Ni yenu. Aminini ya kwamba yanatimia sasa.

83 Sasa, alipoonyesha nguvu Zake kuu duniani, sasa, Yeye hakuwaponya watu mpaka Baba alipomwonyesha kwanza la kufanya. Yohana Mtakatifu 5:19. Alisema, "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Halafu katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Sifanyi neno mpaka nimwone Baba akilitenda kwanza. Lolote Baba anionyeshalo, ndilo Mwana atendalo vile vile." Ni wangapi wanajua Biblia inasema hivyo? Je, mumewahi kusoma hilo katika Biblia? Bila shaka.

84 Sasa, alipofanya jambo hilo, katika safari Yake hapa duniani, alilifanya katika mji mmoja; wakamwamini. Waliponywa, maelfu. Anaenda kwenye mji mwingine, anafanya hivyo; wanaamini. Anaenda kwenye mji Wake Mwenyewe, nyumbani Kwake Mwenyewe; ndipo alipoanza kufanya hivyo, wakasema, "Ni nani Mtu huyu? Alipata wapi hekima hii? Anajuaje jinsi ya kufanya mambo haya? Tunamjua." Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Hakuweza kufanya miujiza mingi kwa sababu ya kutokuamini kwao. Hakuweza kufanya miujiza mingi."

85 Sasa, naomba, kama kuna mwenye dhambi hapa, usiku wa leo, kwamba wakati unapoona, kama Yeye atafanya jambo hilo. Huu ni mji wangu wa nyumbani, na hapa ndipo mahali pagumu zaidi nilipowahi kupigania maishani mwangu. Nimekuwa na

Wahotentoti huko Afrika. Nimekuwa India pamoja na uvuduu na kadhalika, na kupewa changamoto na wachawi wao na kadhalika. Wala sijapata kujisumbua kumfanya Roho wa Mungu kufanya kazi, kama ninavyojisumbua katika mji wangu wa nyumbani. Hiyo ni kweli kabisa. Si kwa sababu watu hawanipendi; kwa sababu, Biblia ni ya kweli. "Amin, amin, nawaambia, kwamba nabii katika nchi yake mwenyewe, akiwa katika jimbo lake mwenyewe, hakosewi heshima, ila katika mahali hapo." Haina budi kuwa hivyo.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tunapoomba.

86 Ewe Bwana mwenye heri, uliyeziumba mbingu na nchi, ukaziumba kwa mkono Wako Mwenyewe uliobarikiwa, ninakuomba Wewe, Bwana, kuwa mwema na mwenye rehema kwetu, usiku wa leo, ukitusamehe dhambi zetu na makosa yetu. Ninakuomba uwe mwema kwa wale walio wagonjwa na wahitaji. Tujalie, Bwana. Na kukiwako na dhambi kati yetu, Ee Mungu wa Milele, uisamehe.

87 Kwa kuwa katika muda mchache tu ujao, Neno Lako ama litapatikana kuwa sawa au lipatikane si sahihi. Ama limepatikana kuwa kweli au ni kosa. Mungu angali ni Mungu, la sivyo Maandiko yamekosea. Na, Bwana, kuhubiri hili, kuliamini, kulishikilia kwenye mashindano ya kuamua, Bwana, ambapo lazima kuwe na jambo litakalotendeka. Lazima kuwepo . . . Ama, Mungu hana budi kujithibitisha Mwenyewe kuwa halisi, la sivyo watu wana haki ya kusema, "Sina budi kuona kwanza."

88 Lakini, Bwana, watu waliozaliwa katika dhambi, wakaumbika katika uovu, kama sisi sote tulivyo, wakaja ulimwenguni wakisema uongo. Ndipo tunajua, Bwana, ya kwamba Mungu mwenye rehema hakika atatuhemu, na atatusaidia, Mungu mpendwa. Tunaomba usiku wa leo kwa ajili ya kila mtu binafsi hapa, ya kwamba Roho Wako atatua juu yao, akitusamehe dhambi zetu na njia zetu mbovu. Na tumtambue Bwana Yesu kama Mwokozi wetu aliyebarikiwa sasa hivi. Na Roho Wake awe mwema.

89 Sasa, Baba, imeandikwa katika Neno, kwa midomo ya Bwana na Mwokozi wetu aliyebarikiwa, Mwanao, ambayo yamesemwa hivi, "Mambo niyafanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya. Yeye aniaminiye Mimi, atazifanya kazi nizifanyazo. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Ulifanya ahadi kwamba wana wa Adamu wasioamini kamwe hawataweza kukuona tena baada ya Wewe kuondoka duniani, bali kwamba Mwaminio angekuona katika nguvu na dhihirisho, katika kila kizazi. Tunaamini hilo, Bwana.

90 Nasi tunaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho za kipindi cha wakati wa Mataifa, ambacho kitamalizika hivi karibuni. Nawe umeiinua miujiza hii mikuu, ili Mataifa wasiwe na udhuru. Umepigwa picha Yako pamoja nasi, kama ile Nguzo kuu ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Na jinsi, ni jambo la ajabu jinsi gani, na kukuona Wewe! Kama ingekuwa ni hiyo picha pekee, "Ni. . ." tungeweza kusema, "vema, huenda ilikuwa ni *hivi-na-hivi*, ingawa ulimwengu wa kisayansi ulisema ilikuwa ni ya kweli." Lakini tunapomwona Roho akishuka na kudhihirisha, na kufanya mambo yale yale aliyofanya, basi hatuna budi kuitambua kuwa ni Bwana aliyefufuka.

91 Tusaidie, usiku wa leo, Bwana. Sisi ni watu wanaoelekea Milele. Tumeelekeza vichwa vyetu kwenye mavumbi ulikotutoa, nasi tuko njiani tukirudi, upesi sana. Wakati huu mdogo wa maandalizi ni kwa ajili ya nafsi zetu. Kuwa mwema sasa, Bwana.

92 Na kama mtumishi Wako anavyosimama, Ee Mungu, pamoja. . .Nina imani ya kuamini ya kwamba Mungu hawezi kusema uongo, ya kwamba atatimiza ahadi Yake. Yeye hana budi kufanya hivyo, kusudi awe Mungu.

93 Bwana, umri wangu unaposonga mbele, wala, sijui ni muda gani zaidi itanibidi kubaki hapa. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utanipa matukio makuu, hata makubwa zaidi kuliko yale ambayo yamefanywa, kama ikiwezekana, ili watu wapate kujua na kujionea kwamba Neno lililo hai la Mungu ni sehemu ya Mungu. Pia jalia kila mtu asiwe na udhuru, usiku wa leo, tunapoondoka hapa, kama wakikupa kisogo. Tujalie. Okoa nafsi na kuwaponya wagonjwa. Kwa maana tunaomba katika Jina la Mtoto Wako, Bwana Yesu, Mwokozi wetu aliyebarikiwa. Amina.

94 Asanteni kwa usikivu wenu. Najua niliwaweka mu—muda mrefu kidogo. Ninalipenda tu Neno hilo zuri la kale. Nilizaliwa ndani Yake. Ninataka kufa pamoja Nalo. Mahali ninapotaka kuenda ni papa hapa nyuma ya jukwaa, ningependa kwenda Nyumbani kukutana na Mungu. Kama ningekuwa na maisha ishirini ya kuishi, ama maisha mia moja, ningetaka kila moja yayo kwa ajili ya Bwana Yesu. Hata kama hakungekuwa na Mbingu ya kwenda, baadaye, bado ningetaka kumtumikia Bwana Yesu, kwa amani na utoshelevu nilio nao wa kujua kwamba Yeye yu hai. Na kwa sababu Yeye yu hai, naweza kuwa hai, pia.

95 Sasa, kama nilisimama hapa, usiku wa leo, kuliambia kundi hili dogo la watu ya kwamba nilikuwa na uwezo wa kumponya mtu fulani, Mimi. . .ninyi mngejua haraka, au watu wanaoijua Biblia, kujua kwamba nitakuwa nikisema uongo. Sina nguvu za kuponya. Wala hakuna mwanadamu yeyote duniani aliye na uwezo wa kuponya. Ni kupitia Kristo pekee, na imani yako katika kazi iliyomalizika. Kwa kuwa kila mwenye dhambi anaweza kuokolewa sasa hivi. Kwa nini? Kwa sababu Yesu

anashuka na kukuokoa sasa? Hapana. Kwa sababu alikuokoa alipokufa kwa ajili yako pale Kalvari. Ulikamilika, mpango mzima wa wokovu, na kwa ajili ya uponyaji wenu. Ni imani yako binafsi kwa Mungu aliye hai.

96 Sasa, nimesimama na Kurani kwenye mkono mmoja, na Biblia kwenye mkono mwingine, mbele ya mamia ya maelfu ya Waislamu, na kusema, "Kimoja hakina budi kuwa cha kweli, na kingine cha uongo."

97 Haijalishi mtu anasema nini, kama hawezi kuunga mkono anachozungumzia, anasema uongo. Na kama Yesu Kristo aliahidi kwamba Kanisa Lake lingefanya jambo lile lile alilofanya Yeye, wala hataliunga mkono, kuna kasoro; Yeye hakuwa Mwana wa Mungu. Lakini kama ataliunga mkono, basi ulimwengu hauna udhuru. Hiyo ni kweli. Anawajibika kulishika Neno Lake.

98 Nawe unawajibika Kwake. Wewe si mali yako mwenyewe. Alikufa ili kukukomboa. Nawe ndiwe anayekutafuta, upate kumrudia Yeye ambaye amekukomboa.

99 Kama ningeweza, usiku wa leo, ningemponya kila mtu hapa ndani. Sina uwezo wa kufanya hivyo. Njia pekee ambayo mhudumu angeweza kufanya hivyo: kuhubiri Neno. "Imani chanzo chake ni kusikia Neno."

100 Nalo Neno pia linasema ya kwamba kutakuwako, katika siku za mwisho, na kote katika nyakati, wakati wa Kanisa, "Kutakuwako, kwanza mitume," ambao ni wamishenari, "pili manabii, na kisha waalimu, halafu karama mbalimbali," zitakuwako Kanisani, kudhihirisha na kuonyesha Uwepo Wake.

101 Sasa, hoja yangu ni hii. Kukiwepo na wageni hapa, siendi kanisani mwangu mara nyingi kutosha kujua ni nani huja hapa. Hii ndiyo maskani ndogo, ninyi wageni, ambamo nime . . . nilimolelewa, maskani yangu ya kwanza na ya pekee. Ni katika mji huu hapa ambapo nimeishi miongoni mwa watu. Ikiwa ninyi ni wageni pamoja nasi, mwulizeni mtu kwenye mji huu, nendeni kwenye kikosi cha polisi, kwa meya wa mji, na mtu yeyote, mpate kujua kama Mkristo yeyote hapa amewahi kuona mojawapo ya maono hayo likishindwa. Haliwezi kushindwa. Ni Mungu. Mnaona? Ni Mungu.

102 Na pale pale mtoni, miaka mingi, mingi, mingi iliyopita, tulipokuwa tukibatiza, kutoka kwenye maskini uamsho wangu wa kwanza, pale ambapo Malaika huyu wa Bwana hapa alishuka, na kuning'inia pale tulipokuwa. Naye akaniambia, "Ujumbe huu utaenea duniani kote, na kuanzisha uamsho utakaoenea kote ulimwenguni, na uwe kabla tu ya Kuja kwa Kristo, mara ya pili."

103 Na wakati Ndugu Davis, Daktari Roy Davis, wengi wenu mnamjua, ambaye alinitawaza kanisani, katika kanisa la Kibatisti. Wakati, alisema niliota ndoto mbaya. Ningewezaje,

nikiwa na elimu ya darasa la saba, kwenda na kuwahubiria wafalme, na watawala, na wafalme, duniani kote? Siwezi kuwaambia. Lakini Mungu alisema hivyo, nami niliamini. Naye amenijalia kuishi kuona jambo hilo, ya kwamba limetukia. Na uamsho mkuu sasa, wa moto wa uamsho, unawaka sasa kwenye kila kilima kote ulimwenguni, tukikungojea Kuja kwa Bwana aliyebarikiwa.

104 Watangulizi wakuu wa mambo haya! Kuna mkimbiaji mkuu ulimwenguni siku hizi: uinjilisti, kama vile Billy Graham; kama Yohana Mbatizaji anayetoka akalime, kisha analiweka shoka kwenye shina la mti, bila kufanya miujiza; wala Yohana hakufanya. Lakini alihubiri Neno.

105 Lakini, mara baada ya yeye kutokea, Bwana Yesu; si mhubiri mkuu hivyo, lakini akifanya ishara na maajabu, akasema, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizifanya zile kazi, msiponiamini Mimi, ziaminini hizo kazi." Kisha akasema, "Sifanyi neno Mwenyewe ila lile nimwonalo Baba akilitenda pia." Naye alifanya nini? Alimwambia yule mwanamke dhambi zake. Alimwambia Filipo mahali alipokuwa kabla Nathanaeli . . . Nathanaeli, mahali alipokuwa, kabla Filipo hajampata chini ya mti, akiomba. Alimwambia Petro jina lake lilikuwa gani. Alimwambia yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu, alipogusa vazi Lake, mambo haya yote.

106 Naye akasema, "Kazi hizi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Nyingi zaidi mtafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu." Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Naye akadhoofika sana. Hakuna mtu mwingine aliyegusa, tujuavyo sisi. Hayo tu ndiyo tuliyo nayo, na Biblia ndiyo tu tunayopaswa kuifuata. Lakini sasa tunaweza kuliona likifanywa, wakati baada ya wakati, na wenye dhambi waliookolewa kwa neema. Kwa nini? Kwa sababu Neno Lake lilisema, "Nyingi kuliko hizi mtafanya." Sasa, Yeye alikufa. Naam, alifufuka tena, Naye yu hai usiku wa leo.

107 Yeye alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Mzabibu hauzai tunda. Huyatakasa matawi, nayo matawi yanazaa tunda. Hana mikono ila yangu na yako. Hana macho ila yangu na yako, kwa sababu amerudi katika Roho.

108 Ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ilikuwa ni Malaika wa Agano, Yesu Kristo. Biblia ilisema hivyo. Msomaji yeyote wa Biblia anajua hilo. Naye akasema, "Ninatoka kwa Mungu. Ninaenda kwa Mungu." Naye akarudi kwa Mungu.

109 Unasema, "Ati alirudi kwenye ile Nguzo ya Moto?" Kabisa. "Je, Biblia inasema hivyo?" Naam, bwana.

110 Paulo, muda mfupi baada ya kufufuka Kwake, alikutana Naye akienda zake Dameski. Ilikuwa ni Nuru ile ile angavu

iliyoyapofusha macho ya Paulo. Wala hakuna mtu aliyeiona ila Paulo. Ilikuwa halisi kwa wengine, na sio kwa wengine.

111 Ninajua, kwa ujuzi fulani, kwamba Bwana Yesu yeye yule hayuko f-. . .hayuko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa hivi. Hiyo ni kweli. Maono yanakuja nawe unaliona.

112 Nayo ilikuwa inang'aa sana hata ikayapofusha macho yake. Akasema, "Bwana! Bwana!"

Akasema, "Mbona wanitesa, Paulo?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu," ile Nuru.

113 Huyu hapa, katika siku za mwisho, akifanya jambo lile lile, matunda yale yale. Roho itajishuhudia yenyewe, kila wakati. Kama atafanya hivyo, usiku wa leo, katika kanisa hili dogo, wakati mnaposimama hapa na miguu pamoja na viungo vinavyouma! Naomba. Ingembidi kulifanya mara moja tu. Mara moja ingetosha.

114 Sisi ni watu ambao tunapapasa gizani. Tunataka kuwazia vinginevyo, lakini sivyo. Tunayaona mambo hayo. Yesu alisema katika Biblia, ama Biblia inazungumza habari Zake, ilisema hivi, "Wana macho, lakini hawawezi kuona; masikio lakini hawawezi kusikia. Ingawa alikuwa amefanya miujiza mingi sana, bado hawangeweza kumwamini." Mnaona ninalomaanisha? Amkeni sasa, upesi.

115 Kama Bwana Yesu atafanya mambo haya, basi Yeye ni Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Na atujalie sasa. Akitujalia, nitamshukuru. Tunapoomba.

116 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, sasa yaliyosalia yako mikononi Mwako, Bwana. Huu ni Ujumbe mdogo, uliovunjikavunjika, kwa shida. Watu wamesumbuka sana roho zao, kwa kusimama, miguu inayouma, na wagonjwa wakilia, na ni kugumu sana. Lakini ninaomba, Bwana, ya kwamba kwa namna fulani ama kwa njia fulani, utawafikishia huo Ujumbe mdogo, kusudi watu walio na imani, wanaoamini kwamba Wewe uliahidi mambo yote yanawezekana.

117 Basi wale waliogusa vazi la Bwana wetu, tunafundishwa katika Agano Jipya, kwamba, "Yeye angali ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Bado anaweza kuzungumza. Angali hai. Nasi ni mzabibu Wake. . .ama matawi Yake ambayo yameunganishwa kwenye Mzabibu. Basi njoo, Roho Mtakatifu, nena na utupe Nuru. Utupe uponyaji. Tupe msamaha wa dhambi zetu, na utufanye kuwa watu Wako. Kwani haya tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa utukufu Wake. Amina.

118 Sijui jinsi tungewasimamisha wagonjwa. Hatuwezi kuwasimamisha wengi mno kwa wakati mmoja. Hebu tuone. Kadi za maombi, je, hivi ninyi nyote. . .Sasa kuna wavulana

wengine wawili ambao wanakuja kutoa kadi za maombi, Gene na Leo. Hawajawahi kufika. Na hawakutoa kadi nyingi sana. Nadhani Billy alikuwa. . . Ngapi? Alikuwa na hamsini tu. Sio lazima uwe nayo. Bila shaka, kuna baadhi tu, zilizochanganywa, tunaweza kuwaleta wachache hapa juu, ha—hadi hapa. Sasa, zilikuwa zipi, kuanzia moja hadi hamsini? Zilikuwa kuanzia moja hadi hamsini. Watafanyaje? Wanashuka moja kwa moja na kuzichanganya kadi, kati yenu.

119 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ili tu kuzungumza nanyi, kuwasiliana tu. . . Hapa, simama *hivi*, maana ninaamini sauti haiingii vizuri sana kwenye maikrofoni hii ndogo hapa. Ikiwa mtaninii. . .

120 Ikiwa Roho Mtakatifu atafunua kile kilichokuleta hapa, kama yule mwanamke kisimani, aliyemjia Bwana Yesu. Naye Yesu akasema, "Mambo haya niyafanyayo ninyi nanyi mtayafanya." Na kama atafunua unachotaka Kwake, chochote unachotaka, kilicho shida yako, je, ungeamini ilikuwa ni Yeye? Ungeamini. Wangejua ingebidi itoke kwenye nguvu za kimbinguni. Sasa kama huyu mama. . .

121 Kama ningesema, "Mama, unataka—unataka pesa kwa sababu wewe—wewe ni. . . una deni la kulipa. Utazipata." Huh! Angekuwa na haki ya kutilia hilo shaka. Kama ningesema, "Wewe ni mgonjwa na utapata afya." Angekuwa na haki ya kutilia hilo shaka. Asingejua.

122 Lakini vipi kama Roho Mtakatifu akirudi kule chini, na kuonyesha jambo fulani ambalo amekuwa akifanya? Kitu ambacho atajua kama hiyo ilikuwa kweli au la. Atakuwa mwamuzi wa hilo. Mnaona? Mwache awe mwamuzi. Unaona?

"Sasa, ati unasema unafanya nini, Ndugu Branham?"

123 Baada ya kuhubiri namna hiyo, na katika kanisa langu la nyumbani hapa, ninangojea upako huo ushuke, yule Roho Mtakatifu mbarikiwa atie upako. Nami natumaini ya kwamba atatia, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

124 Sasa hebu huyo mama. . . Yuko hapa. Ameinamisha kichwa chake. Macho yake yamefumbwa. Yuko katika maombi. Nataka uombee chochote unachotaka. Naye Bwana akifunue, nawe uwe mwamuzi.

125 Huyu mwanamke, ikiwa kusanyiko bado linaweza kusikia sauti yangu, anasumbuliwa na ugonjwa mbaya sana wa fadhaa. Nami ninamwona daktari akifanya kitu fulani. Anauzungushia mkono wake ki—kitu fulani. Kisha anasema ana shinikizo kuu la damu. Hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli, mama? [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Sasa jambo fulani. . .

126 Ulisikia sauti hiyo? Hiyo haikuwa ni mimi. Sikuwa na uhusiano wowote na hiyo. Sasa, kadiri ninavyozungumza naye, ndivyo mengi yangetokea. Tazameni tu sasa, tutazungumza

naye tena. Sijui alichosema shida yake ilikuwa. Ikiwa wao... Ilivyokuwa, itakuwa kwenye kanda kule nyuma, mnaona. Lakini, chochote kile, ni kweli.

127 Sasa hebu tumwangalie tena. Naam, sasa ninamwona katika ugonjwa wa fadhaa. Na damu yake ina kasoro. Wala hatoki kwenye mji huu. Anatoka Louisville. Naye amekuwa hospitalini hivi majuzi, na ilikuwa ni kwa ajili ya nimonia. Naye daktari wake anamwambia kwamba imeibuka tena, na hana budi kurudi tena hospitalini. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli.

128 Lakini sio lazima urudi, mama. Imani yako imekuponya. Wewe u—umeponywa sasa, katika Jina la Bwana Yesu. Sasa, nenda ukapone. Bwana akubariki.

Je, nilikuwa na uhusiano wowote na hilo? Hata kidogo.

129 Sasa, huyu hapa amesimama mama ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu. Nadhani hatufahamiani. Sivyo? Uliniona, lakini labda sijawahi kukuona. Pengine ulikuwa kwenye mikutano fulani au mahali fulani. Sasa, kama Bwana Yesu atanijulisha kilichokuleta hapa, ungejua basi, bila mimi kukujua wewe, kwamba kuna njia fulani niliyo nayo ya kujua. Itabidi ujue kuwa inakuja kwa njia ya kimbinguni. Basi ungefikiri ingekuwa ni nini? Jambo lile lile ambalo Biblia ilisema, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele.

130 Mngeamini hivyo enyi kusanyiko? Huu hapa mkono wangu. Nijuavyo mimi, sijawahi kumwona mwanamke huyu maishani mwangu. Mnaona? Naye aliniona...

131 Lakini sijui uko hapa kwa sababu gani. Sijui lolote kuhusu hilo. Si—si—sijui tu, lakini Mungu anajua. Sasa, kama Bwana atalifunua, amina. Hayo tu ndiyo angeweza kufanya kama Yeye alisimama hapa. Kama ni kwa ajili ya uponyaji ama chochote kile, Yeye anataka tu uamini, hivyo tu. Hii ni kudhihirisha kwamba Neno Lake ni kweli.

Kitu fulani kilitokea kwenye kusanyiko basi. Iweni tu na imani.

132 Sasa inaonekana kwamba kuna...Sasa kama ungeweza kuona kati yangu na huyu mwanamke. Unasumbuliwa na udhaifu. Una vipindi vya udhaifu kweli. Hiyo ni kweli. Udhaifu mkubwa tu; fadhaa, udhaifu. Lakini hiyo siyo sababu yako ya kuwa hapa. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, na huyo ni mwanamume. Ni mume wako. Asingeweza kuja, kwa sababu ana tatizo kubwa la moyo na fadhaa. Nawe hutoki kwenye mji huu. Unatoka mahali panapoitwa Columbia. Columbia, Kentucky. Jina lako ni Lottie Goodin. Jina la mume wako, Elmer. Nenda zako nyumbani upate kama ulivyoamini. Na Mungu akujalie hilo, katika Jina la Bwana Yesu.

Amini tu. Amini. Usiwe na shaka sasa. Amini tu.

133 Nadhani hatufahamiani, bwana? Sasa, hawa hapa wanaume wawili. Kama vile tu Filipo alivyoenda akamkuta Nathanaeli, na kumleta kwa Bwana. Sikujui, wala hunijui mimi. Ila Mungu anatujua sote. Unafahamu kuwa kuna kitu kinachoendelea sasa hivi. Unaona? Kusimama mbele ya mtu kusingekufanya ujisikie hivyo, hisia hiyo nyenyekevu, tamu.

134 Sasa, laiti mngeweza tu kuona Nuru inayojongea, ikitua kati yangu na huyu mtu. Sasa ananiondokea. Wala hayuko hapa kwa ajili yake mwenyewe. Yuko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni jamaa, mpwa. Naye yuko katika jeshi, katika jeshi la wanamaji. Lakini hayuko mbali na hapa. Yuko karibu na mahali ambapo kuna mambo mengi ya kijeshi. Ni hospitali, na ni Fort Knox. Naye ni kipofu, kutokana na ma—marisawa. Naye daktari anasema hakuna tumaini kwake. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Basi na iwe kulingana na imani yako, ndugu yangu. Basi pokea, katika Jina la Bwana wetu Yesu. Amina. Unaamini? Mungu akubariki, ndugu yangu mpendwa.

Wewe, mtu anayefuata. U hali gani? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

135 Jinsi Mwokozi wetu mbarikiwa anavyopendeza, jinsi—jinsi alivyo kila mahali, jinsi ambavyo Yesu yeye yule aliyesimama Galilaya!

136 Ngoja kidogo. Je, mtu huyo alikuwepo, hapo, jukwaani sasa hivi? Alikuwa ni nani kati ya hao watu? Mtu huyo hapo? Vema. Mwaweza kuketi.

137 Ni huyu mama papa hapa mwishoni, mwenye kofia nyekundu. Naam. Unamwombea rafiki ambaye ni mlevi sugu. Hiyo ni kweli. Vema. Ikiwa unaweza kuamini, unaweza kupokea. Amina. Vema.

138 Je, utaamini? Sikujui wewe. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hatufahamiani. Lakini ikiwa Bwana Mungu wa Mbinguni atajidhihirisha Mwenyewe, katika uweza Wake, na kufunua ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, utamwamini? [Dada huyo anasema, "Ninamwamini."—Mh.]

139 Hebu tuone, ni hawa watatu au . . . watu au . . . Kumekuwa na zaidi ya hao waliopitishwa, sivyo? Tatu ni thibitisho, bila shaka. Lakini, chochote kile.

140 Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ndiyo shauku yako kuu. Na hiyo ni kwa ajili ya mwanaume. Na mtu huyo ni mwanao. Naye ana shida ya moyo. Na amekuwa na aina fulani ya jambo fulani lililomtokea. Ni kiharusi. Na kimempoozesha kwa sehemu. Nawe pia ni mgonjwa. Una uvimbe wa utumbo mpana. Ni ugonjwa wa matumbo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

141 Na jambo lingine, ninamwona mjumbe akienda mahali mahali. Hapana. Ilikuwa ni mtu fulani aliyekuja hapa

maskanini, wakati fulani uliopita, na kuomba maombi kwa ajili yako, naye Bwana akakuponya. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mikono yako. Unaamini utapata unachoomba? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Basi na iwe kwako, dada yangu, kama Bwana Yesu alivyotoa. Amina.

U hali gani?

142 Je, kila mtu anaamini? Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa amini. Ni nini?

143 Inabidi tu nizungumze hapa kwa sekunde moja tu, tafadhali, maana nina wengi zaidi wa kuwafikia, nami ninataka tu kupumzika kwa muda kidogo tu. Hamtambui kile hilo linachokufanyia. Ni mbaya kuliko kuombe-. . .Hakika. Ni wangapi wanaokumbuka, yule nabii mkuu Danieli aliona ono moja naye akafadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi? Mnakumbuka? Hakika. Mnaona? Ni neema Yake tu.

144 Sasa ninyi huko nje, ambao hamko kwenye mstari wa maombi, anzeni tu kuangalia huku. Mimi. . .Mnasema, "Ndugu Branham, hilo lingefaa kitu?" Hakika. Mwombe tu Bwana Yesu. Useme, "Baba mbarikiwa, jalia niguse vazi Lako. Na njia pekee ninayojua ya kwamba ulinigusa, ama ulinisikia, iwe kwamba kama utanena kupitia midomo ya mtu huyo na kuniambia ninachoomba, kama vile huko juu jukwaani. Nakuamini." Ninyi msio na kadi za maombi sasa, ombeni na muamini hivyo. Msiwe na shaka. Iweni tu na imani.

145 Sasa, huyu ndiye mgonjwa, Ndugu Neville? Huyu ndiye mgonjwa? [Ndugu Neville anasema, "Naam, ndiye."—Mh.]

146 Sikumaanisha kukuacha usimame hapo. Lakini ni. . . Unaweza kuwazia yanayotukia. Hivi hatufahamiani? [Dada huyo anasema, "Kweli."—Mh.] Hatufahamiani. Sasa hebu hili litatuliwe. Simfahamu mwanamke huyu. Simjui. Sijawahi kumwona, maishani mwangu. Na hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. Hiyo ni kweli. Mara ya kwanza tumewahi kutupiana macho. Naye ni mwanamke tu aliyekuja hapa jukwaani. Mtu fulani alimpa kadi ya maombi, naye akaja tu hapa jukwaani. Hilo tu ndilo ninalojua juu yake.

147 Lakini Bwana Yesu anaweza kulifunua. Na kama anaweza kulifunua, basi Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hivyo ndivyo hasa Yeye alivyoahidi kufanya. Na kama ahadi hiyo imetimizwa, Yeye atatimiza kila ahadi aliyotoa. Naye aliahidi kukuponya ikiwa utaamini. Unaona ninachomaanisha sasa? Haiwezi kushindwa. Haina budi kuwa hivyo. Loo, Jina Lake libarikiwe! Kamwe hawezi kushindwa.

148 Ikiwa Bwana Yesu atanijalia kujua kile kimekuwa maishani mwako, hakika atajua kitakachokuwa maishani mwako. Wewe kuwa mwamuzi wa hilo.

149 Ni wangapi wangesema, "Nitaamini kwa moyo wangu wote, kama mwanamke huyo atainua mikono yake, nyote wawili mseme hamjawahi kukutana hapo awali, na Bwana Yesu atalifunua, nitaamini"? Kwa—kwa moyo wako wote, utafanya hivyo?

150 Mungu hataki tuwe wavivu. Anataka tuwe na imani. Sisi hapa, mbele ya mimbara, Biblia iko hapa, na, sote wawili, tumesimama hapa.

151 Mama huyo anasumbuliwa na ugonjwa mbaya sana wa fadhaa. Hiyo ndiyo shida yako. Lakini unachofikiri ndicho, ni kitu fulani tumboni mwako, ambacho kinakupa gesi tumboni mwako. Hiyo ni mishipa inayofanya hivyo. Hiyo ni kweli. Pia una kasoro shingoni mwako, na mabegani mwako. Kwa sababu. . . Unaenda kanisani, nawe ni Mkristo. Nawe ni mpiga kinanda kanisani mwako. Na unapocheza piano, mateso hayo yanakusumbua unapocheza piano. Hiyo ni ROHO ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Nawe hutoki kwenye mji huu. Lakini unatoka katika mji ulio mtoni. Na sio Louisville. Ni Cincinnati. Cincinnati, Ohio. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

152 Je, unaweza kuona mstari huo? Imani iligonga papo hapo, maana ninii yake. . . Huyo jamaa mdogo anayeketi papo hapo, kidogo ana nywele za mawimbi, ana uhusiano na wewe. Hiyo ni kweli, kijana. Imani yako iligusa kitu fulani. Unasumbuliwa na ngiri. Hiyo ni kweli. Nawe pia unatoka Cincinnati. Hiyo ni kweli. Unaamini?

153 Maskini msichana mmoja aliinua mabega yake, akiketi papa hapa, akiwa na kofia ya waridi, amejizungushia shela. Ana matatizo na macho yake. Hiyo ni kweli. Naye anatoka Cincinnati. Hiyo ni kweli. Na hebu nikwambie. Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Unaamini? Unamwombea mume ambaye ameanza kunywa pombe. Alikuwa akienda kanisani na kuwa Mkristo, lakini amerudi nyuma, naye anakunywa sasa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Vema, inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Kwa hiyo, sawa.

154 Maskini huyo msichana anayeketi karibu nawe hapo, anaugua ugonjwa wa fadhaa. Yeye pia anatoka huko juu. Lakini jambo unalohitaji zaidi kuliko hapo awali. . . Unaenda kanisani, lakini bado hujawa Mkristo halisi. Hiyo ni kweli. Je, utamkubali sasa kama Mwokozi wako binafsi, kwa kuwa Yeye yuko? Iwapo unamkubali, mpungie mkono wako, sasa umkubali. Mungu akubariki. Dhambi zako zimesamehewa. Nenda kwa amani, na fadhaa yako imetoweka. Amina. Nenda nyumbani na uwe mwenye furaha, katika Jina la Bwana.

Unaamini? Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.

155 Sasa nilihisi mtetemo huko nyuma. . . si mtetemo, bali roho isemayo ninasoma mawazo yao. Sifanyi hivyo. Kuwa mwangalifu, hiyo itakuja kwako.

156 Hapa, mtu huyu hapa, weka mkono wako juu ya wangu, bwana. Hata sitakutazama. Ikiwa Bwana Yesu atanifunulia shida yako ni ipi, utakubali uponyaji wako ama chochote unachohitaji? Je, utaukubali? Mtu huyu hapa, utaukubali? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Ugonjwa wa moyo. Sasa, nenda ukaponywe. Bwana Yesu akuponya. Ikiwa unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda na kuwa mzima. Mungu akubariki.

157 Njoo. Sasa, mama huyu hapa. Huyu mwanamke ana roho ya mauti juu yake, kwa kuwa ana kansa. Unaamini Bwana atakuponya, dada? [Dada huyo anasema, "Hakika ninaamini."—Mh.]

158 Ewe Mungu mpendwa, uliyeziumba mbingu na nchi, maskini mwanamke huyu amenaswa katika makucha ya ibilisi. Kivuli cheusi kinaning'inia karibu, lakini tunampa changamoto pepo huyu. Katika Jina la Bwana Yesu, toka kwa huyo mwanamke, na hebu aende akapone, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Bwana akubariki, dada. Nenda, wala usiwe na shaka kwa chochote.

159 Kama unaweza kuamini! Je, unaamini? Amini tu. Biblia ilisema, "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Lakini ndivyo tu linavyoweza kufanywa.

160 Hatufahamiani, bwana, lakini Bwana anatujua sote wawili. Kama atanifunulia kile kilichokuleta hapa, je, utakipokea? Una ugonjwa wa tumbo.

161 Na jambo lingine, wewe ni mwenye dhambi. Hujamkubali Bwana kama Mwokozi wako. Je, utamkubali kama Mwokozi wako? Mwinulie mikono yako, mkubali Yeye kama Mwokozi wako, nami nitakutangazia, katika Jina la Kristo, umeponywa ugonjwa wako wa tumbo. Nenda wala usitende dhambi tena. Amina.

Uturehemu, Mungu uliye hai!

162 Je, unaamini Mungu anakuponya na ugonjwa huo wa moyo? Basi nenda huko nje upate kuwa mzima, katika Jina la Bwana Yesu.

163 Je, maskini mama huyu anayeketi hapa, aliyevaa koti jeusi, miwani, una kadi ya maombi, mama? Huna? Una shida masikioni mwako, unataka niiombee. Tena una tatizo la matumbo, pia. Je, hiyo ni kweli? Vema. Limekwisha sasa. Nenda zako, amini. Kama unaweza kuamini!

164 Unataka maombi kwa ajili ya mtu fulani, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Dada, katika hospitali ya wendawazimu.

165 Ee Mungu wa Milele, tuma baraka Zako kwa mtu huyo, na jalia aponywe. Tujalie, Ee Bwana, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Yakute kama ulivyoamini, ndugu yangu. Usiwe na shaka.

166 Kama unaweza kuamini! Je, mnaamini? Loo, ungeweza kuwa wakati mtukufu jinsi gani kwa wote, kama mngeninii . . .

167 Inaonekana kuna Nuru karibu na yule mwanamke ambaye kwa namna fulani ni mnene, akinitazama, papa *hapa*. Ni yule mama aliye ndani. Inatoka kwake, kwa sababu mama huyu ameponywa hivi punde. Lakini huyo mama mwingine ana kitu fulani, kitu kama shinikizo la damu, shinikizo dogo la damu. Unaamini Bwana atakuponya, mama? Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Unaamini, mama, unayeangalia karibu na hapo? Ukiamini kwa . . . Unaamini, kwa moyo wako wote? Naam. Unakubali? Vema. Unaweza kwenda na ukaponywe, katika Jina la Bwana Yesu.

168 Mtu anayeketi papa *hapa*, akiomba. Unataka nikwambie unachosema? "Bwana, niponye uvimbe huo wa puani." Vema. Anakuponya, katika Jina la Bwana Yesu, kama unaweza kuamini.

169 Unaamini Mungu atakuondolea ugonjwa huo wa moyo, unaweza kwenda kuwa mzima? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.]

170 Ee Bwana, tuma rehema Zako na nguvu, na umbariki maskini mtu huyu, Bwana. Na kumponya, kupitia Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

Amini sasa. Usiwe na shaka. Mambo yote yanawezekana.

171 Yabisi kavu si kitu kibaya kwa Mungu kuponya. Unaamini ya kwamba ataiponya?

172 Ee Bwana, naomba, kwamba, katika Jina la Yesu, kwamba utamtuma Roho Wako juu ya mwanamke huyu mpendwa na kumponya kabisa. Na jalia aende nyumbani kwake, akishangilia, na aponywe. Bila shaka hata kidogo, lakini nikiamini kwamba inafanyika hivi sasa. Naye atapata alichoamini. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

173 Je, unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kupata kile unachoomba, basi.

174 Huko nyuma kabisa, pembeni, huyo hapo Malaika wa Bwana amesimama huko nyuma, Nuru. Kama unaweza kuamini! Wewe hapo, kama safu tatu upande huu wa nyuma. Vizuri kabisa ninavyoweza kuona kutoka hapa, ni yapata mtu wa pili ndani; anayeomba huko nyuma, ambaye yuna ugonjwa wa matumbo. Je, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema. Unaweza kupata kile unachoomba.

175 Weka mikono yako juu ya mtu huyo aliye karibu nawe hapo. Kwa maana, anaomba, mwenye ugonjwa wa mafindofindo. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile unachoomba. Amina.

176 Mnaamini? Bwana Yesu, moja kwa moja kwenye ninii Yake…wakati huu, anaweza kumfanya kila mmoja wenu kuwa mzima kabisa, kama mnaweza kuamini jambo hilo. Je, mnaamini? Basi wekeaneni mikono, kwa dakika moja tu, nami nitawaonyesha utukufu wa Bwana.

177 Sasa, ama Ndugu Wood, au Billy, mmojawapo, ananigusa mgongoni, ambalo najua umefika wakati ambao hawataniruhusu kusimama muda mrefu zaidi, kwa sababu nguvu zangu zimeisha.

178 Nilisema, muda mfupi tu uliopita, kama Mungu angekuja na kujidhihirisha Mwenyewe, kama angethibitisha, kwa tukio fulani, ya kwamba Yeye ni Bwana Mungu, ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, basi hamngekuwa na sababu yoyote ya kutilia shaka; wala haingewezekana, katika Ujumbe wangu usiku wa leo, kwa yeyote wa wale ambao wamewahi kuuona Uwepo wa Mungu. Filipo angewezaje kushuku? Nathanaeli angewezaje kushuku? Yule mwanamke aliyetokwa na damu angewezaje? Asingeweza kutilia shaka. Alikuwa amemgusa, Naye alikuwa amemfunulia kile kilichomfanya amguse.

179 Usiangalie ukubwa wa kanisa au jinsi linavyoonekana. Usiangalie hili kusanyiko dogo, kwa sababu sisi sote ni watu wa kawaida. Bali mfikirie Bwana aliyebarikiwa, ambaye Uwepo Wake upo hapa, Yule anayejionyesha Mwenyewe hai. Wewe mwamini sasa hivi, nawe unaweza kupata chochote unachoomba, na kuamini. Sasa Yeye anaweza kuponya papa hapa vivyo hivyo. Uwepo Wake…Tayari umeponywa. Kuna kitu kimoja tu kinachokuzuia usiupokee, hicho ni kutokuamini. Kiondoe hicho, sasa hivi. Usikose kuamini tena; kitupilie mbali, na umkubali Bwana Yesu kama mponyaji wako. Tazama kitakachotendeka. Toka nje ya jengo hili, ukishangilia, kwa kuwa sasa hivi uko Mbele za Bwana Yesu. Si kwa sababu uko katika maskani hii, bali kwa sababu Yeye amekuja na kututembelea. Si kwa sababu mimi ndiye mhubiri, au hili… ama Ndugu yangu Neville, ama yeyote wa hawa Wakristo wengine, si uwepo wetu, bali ni Uwepo Wake. Hauwezi kukosea. Ni Biblia. Ni Ukweli. Jina Lake lihimidiwe!

180 Licha ya Yeye kusema, "Katika nchi yetu wenyewe, miongoni mwa watu wetu wenyewe," neema imelishinda, usiku wa leo, kwa sababu ya kukaribia kwa wakati. Mwisho umekaribia. Aliahidi ya kwamba wakati mambo haya yatakapoanza kutukia, ya kwamba wakati wa mwisho ulikuwa umekaribia.

181 Amini sasa ninapoomba. Biblia ilisema, "Kuomba kwa bidii kwafaa sana." Basi na tuombe, mnapoombeana, huku mkiwekeana mikono.

182 Bwana, umekuwa maficho yetu katika kila kizazi. Umekuwa kimbilio letu. Tumekungoja Wewe kwa muda mrefu. Kwa

muda mrefu kanisa hili la kiprotestanti limetamani kuona siku ambayo lingeweza kusimama kwa miguu yake. Wakati kundi dogo ambalo limesukumizwa upande mmoja, kwa sababu hawangepatana na kutokuamini kwa wasioamini ambao wamejifunga nira. Nao walitoa changamoto yao kwamba ule Moto mdogo ulioanza kushuka, miaka michache iliyopita, hatimaye utazimika. Lakini, loo, tuna furaha sana kwa ajili ya Kapteni wetu mkuu, Daudi, ambaye anasimama katikati yetu usiku wa leo, na kumpa adui changamoto.

183 Ee Bwana Mungu, tungeomba maombi haya ya imani kwa kila mtu hapa. Wajalie wajue, kwa wakati uu huu, ya kwamba Uwepo Wako mkuu upo hapa, kupitia upesi juu ya kusanyiko hili lote na kumponya kila mtu. Ee Roho Mtakatifu mkuu, huenda kila moyo umesisimkwa wakati huu, anapowabatiza katika Uwepo mkuu wa Roho Mtakatifu.

184 Loo, Shetani, umeshindwa. Toka mahali hapa na upate kutoka kwa watu. Katika Jina la Yesu Kristo, kila mtu na aponywe.

185 Ee Mungu wa Milele na mbarikiwa, tujalie mambo haya kupitia Jina la Yesu Kristo.

186 Kila mtu anayeamini kwamba umeponywa, simama kwa miguu yako na umpe Mungu sifa. Asanteni, na Bwana Mungu awabariki! Ndugu Neville.

57-1229 Imani
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org